TRC
TANZANIA RAILWAYS CORPORATION

# RELI NA MATUKIO GAZETI

Kila Mwezi





Agosti 22, 2019

Gazeti la Reli | Toleo Namba 1 | Habari | Makala | Matukio | Picha



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli akipata Maelezo kuhusu maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa alipotembelea Banda la TRC katika maonesho ya SADC katika kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha J.K Nyerere.

## TRC YASHIRIKI MAONESHO YA NNE YA WIKI YA VIWANDA YA JUMUIYA YA MAENDELEO YA KUSINI MWA AFRIKA - SADC

Shirika la Reli Tanzania – TRC lashiriki Maonesho ya 4 ya Viwanda na Biashara ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika – SADC katika kituo cha mikutano cha kimataifa cha J.K Nyerere jijini Dar es Salaam tarehe 05 – 06 Agosti 2016.

Maonesho ya Viwanda na Biashara huduma pamoja na fursa zilizopo katika jumuiya ya SADC zikiwemo biashara, uwekezaji na ukuzaji uchumi.

>> Inaendelea Uk. 2

### Historia yaandikwa kurejea kwa safari za treni Dar - Tanga - Kilimanjaro



>> Uk. 3

### TRC, WFP, URC, TPA na MSCL waadhimisha mwaka mmoja wa Mafanikio



>> Uk. 4

### Ujenzi wa Mahandaki ya SGR waanza rasmi Mkoani Morogoro



>> Uk. 5

# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA NNE YA WIKI YA VIWANDA YA JUMUIYA YA MAENDELEO YA KUSINI MWA AFRIKA - SADC

>> Inatoka Uk. 1

Mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alifungua rasmi maadhimisho hayo na mkutano wa wakuu wa nchi za SADC Agosti 5, 2019.

Aidha Rais Magufuli alipata fursa ya kutembelea banda la Shirika la Reli Tanzania – TRC katika maadhimisho ya maonesho ya 4 ya viwanda na biashara ya Jumuiya ya maendeleo ya kusini mwa afrika - SADC

Naye Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa atembelea Banda la Shirika la Reli Tanzania – TRC katika maadhimisho ya maonesho ya 4 ya viwanda na biashara ya Jumuiya ya maendeleo ya kusini mwa afrika - SADC ambazo ni nchi 16 yaliyofanyika katika kituo cha mikutano cha kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Agosti 6, 2019.

Aidha, waziri mkuu ametoa pongezi za dhati kwa shirika la Reli nchini kwa usimamizi mzuri wa mradi mkubwa wa kitaifa wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR unaoendelea nchini “TRC inaonekana mmejipanga vizuri“ waziri Majaliwa alisema.

Katika maonesho hayo jumla ya nchi 16 za jumuiya ya maendeleo ya kusini mwa afrika (SADC) zimehudhuria ambazo ni Tanzania, DRC Congo, Angola, Lesotho, Malawi. Madagascar, Mauritus, Mozambique, Namibia, South Africa, Seychelle, Swaziland, Zimbabwe, Zambia na visiwa vya Comoro.

Maonesho ya SADC yamewasaidia wananchi wa Tanzania na wageni wa nchi za kusini mwa Afrika kupata fursa mbalimbali ikiwemo kujua miradi mikubwa ya kitaifa ya kimkakati inayosimamiwa na Shirika la Reli Nchini ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa SGR awamu ya kwanza Dar es Salaam – Morogoro ambapo ujenzi umefikia asilimia 60. Awamu ya pili ya ujenzi Morogoro – Matukupola ambapo ujenzi umefikia zaidi ya asilimia 14 pia Shirika linasimamia mradi wa uboreshaji wa reli ya kati Dar es Salaam Mpaka Isaka Km 970 –TIRP ambao ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 34 na ufunguzi wa njia ya Reli ya Tanga, Moshi na Arusha mwishoni wa mwezi wa saba.

Maonesho haya ya viwanda ni fursa kwa Shirika la Reli Nchini kwani kupitia sekta ya uchukuzi na usafirishaji kwa njia ya reli itaongeza wigo wa masoko ya ndani na nje ya nchi. Reli hii ya kisasa itayojengwa itakuwa na faida kubwa kiuchumi nje na ndani ya nchi kwani itachochea maendeleo katika sekta ya kilimo, viwanda, biashara na madini hususani maeneo ambayo reli itapita pamoja na nchi jirani hasa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo.



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Shirika la Reli Tanzania - TRC Bi. Jamila Mbarouk akifafanua kuhusu maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR alipotembelea Banda la TRC katika Wiki ya Maonesho ya Viwanda na Biasahara yanayofanyika katika Kituo cha Mikutano cha J.K Nyerere jijini Dar es Salaam Agosti 05 - 09, 2019.

# HISTORIA YAANDIKWA KUREJEA KWA SAFARI ZA TRENI DAR - TANGA - KILIMANJARO

>> Inatoka Uk. 1



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muunganowa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amefanya ufunguzi wa njia ya reli ya Tanga mpaka Moshi mkoani Kilimanjaro katika hafla iliyofanyika mjini Moshi , Kilimanjaro hivi karibuni Julai 2019, iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wa vyama pamoja na wa dini.

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa amelipongeza Shirika la Reli Tanzania -TRC kwa Kurejesha njia ya Tanga-Moshi ambayo takribani zaidi ya miaka 12 ilikuwa haifanyi kazi. Waziri Mkuu amesema kuwa mafanikio haya ni utekelezaji wa sera ya kitaifa na Mkakati wa Nchi kuinua sekta mbalimbali za kimkakati ili nchi ya Tanzania ifikie Uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Waziri mkuu aliongeza kuwa juhudi na kujitoa kulikofanyika kurejesha njia ya reli kuanzia Dar es Salaam hadi Tanga na kisha kuelekea Moshi ,Kilimanjaro ni uamuzi wa busara uliokuja kwa wakati na unaoshamirisha azima yetu ya kuchochea ukuaji wa uchumi lakini na kuyabadili maisha ya wananchi kupitia huduma bora za usafiri na uchukuzi .

" Kamwe hatuwezi kufikia hadhi hiyo muhimu kiuchumi bila kuwa na miundombinu imara ikiwemo ya reli " amesema Mhe. Kassim Majaliwa.

Aidha Waziri Mkuu amebainisha kuwa Tanzania inapakana na nchi zaidi ya tano ambazo zinategemea sana miundombinu ya nchi ya Tanzania ya usafirishaji na uchukuzi ndani ya nchi ili kupitisha bidhaa. Pia aligusia juu ya mradi mkubwa wa kihistoria wa SGR unaoendelea kuanzia Dar es Salaam hadi Mokutopola na kusema kuwa Serikali ya awamu ya tano imewekeza takribani Shilingi Bilioni 7.2 fedha za walipa kodi kutekeleza mradi huo .

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Atashasta Nditiye ameipongeza Serikali ya awamu ya tano kwa kutoa fedha pia amepongeza bodi na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania katika ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya ufufuaji wa Shirika na njia mbalimbali za reli zilizokufa kwa miaka kadhaa. Pia Naibu Waziri ametoa rai kwa wafanyazi wa TRC na watanzania wote kuwa walinzi wa miundombinu ya reli ambayo ni kichocheo kikubwa cha uchumi wa nchi yetu.

> **"TRC imepewa dhamana na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusimamia uhuishaji na utendaji wa shirika pamoja na kuboresha huduma za reli " Mhe . Atashasta Nditiye**

## TRC, WFP, URC, TPA NA MSCL WAADHIMISHA MWAKA MMOJA WA MAFANIKIO

>> Inatoka Uk. 1

Shirika la Reli Tanzania – TRC, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani – WFP, Mamlaka ya Bandari Tanzania – TPA, Shirika la Reli Uganda – URC pamoja na Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania – MSCL waadhimisha mwaka mmoja wa mafanikio katika usafirishaji wa Mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam, Mwanza hadi Portbell nchini Uganda kupitia Ziwa Victoria hivi Karibuni Julai 2019.

Usafiri wa reli kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi Portbell nchini Uganda kupitia reli ya kati kwa ushirikiano wa TRC, TPA, MSCL, URC na WFP umezidi kuimarika tangu kurejeshwa kwa safari hizo mwezi Julai 2018 ambapo Shirika la Mpango wa Chakula Duniani limesafirisha jumla ya Tani 36,000 hadi kufikia mwezi Julai 2019.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe amethibisha hilo alipokuwa akihutubia hafla fupi ya kuadhimisha mwaka mmoja wa mafanikio hayo katika Bandari ya Mwanza Kusini jijini Mwanza kabla ya kuanza kwa safari ya 14 ya Meli ya MV Umoja inayobeba shehena ya Chakula pamoja na Mizigo mingine kuelekea Portbel nchini Uganda na hatimaye hadi Sudani Kusini.

Hafla ilihudhuriwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Isack Kamwelwe, Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Innocent Bashungwa, Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi Dkt. Leonard Chamuriho, Wakuu wa Mikoa ya Geita na Mwanza, Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu TPA Mhandisi Deusdedith Kakoko, Mwakilishi Mkaazi WFP Bwana Michael Danford, Kaimu Mkurugenzi wa MCSL Mhandisi , wafanyakazi, viongozi wa chama na serikali, wanahabari pamoja na wananchi.

Akizungumza katika hafla hiyo Waziri Kamwelwe anesema kuwa`usafiri wa reli na meli ni nafuu zaidi kuliko aina nyingine za usafiri

"Tafiti zimebainisha kuwa usafirishaji kwa njia ya reli na meli ni usafiri wa uhakika na wenye gharama nafuu hususani kwa mizigo inaykwenda umbali mefu ukilinganisha na aina nyingine za usafiri, mfano takwimu za WFP zinaonesha kuwa zimepunguza gharama za usafirishaji kwa 40% kwa kutumia njia hizi za usafiri" Alisema Waziri Kamwelwe

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa amesema lengo kuu la safari hii ni kuutangaza ushoroba wa kati kwa wafanyabiashara na wateja kwa ujumla kwa kuwa njia hiyo inaokoa muda na gharama za usafirishaji

"WFP tangu waanze kutumia usafiri wamepunguza gharama kwa 40%, Unapotumia reli unakuwa na nafasi nzuri ya kupanga bei ya bidhaa kwa unafuu, pia kwa kutumia njia hii mfanyabiashara atapunguza zaidi ya siku nne kusafirisha mzigo hadi Uganda" alisema Kadogosa

Hafla hiyo iliambatana na safari kuanzia Bandari ya Mwanza Kusini hadi Bandari ya Portbell na kupokelewa na wenyeji ambao ni



Waziri wa Uchukuzi nchini Uganda Mhe. Edward Katumba Wamala na Maafisa wa Shirika la Reli Uganda ambapo timu ya maafisa wa URL, TRC, WFP, TPA na MSCL walipata fursa ya kutembelea Bandari ya Jinja nchini Uganda kwa lengo la kuendelea kuimarisha huduma za usafiri wa reli kutoka Mwanza hadi Bandari ya Jinja kwa kuifufua bandari hiyo pamoja na miundombinu ya reli ili kufungua safari za Mizigo kutoka Mwanza hadi Jinja.

Akizungumza na TRC Reli TV Charles Ruzigye Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Meli Shirika la Reli Uganda amesema kuwa URC kwa kushirikiana na TRC, TPA, MSCL na WFP tumepanga kurudisha huduma ya usafiri kutoka Mwanza hadi Jinja kwa kufungua njia ya reli ya pamoja na Bandari ya Jinja.

"Mpango ni kupanua bandari pamoja na kukarabati reli kutoka Bandari ya Jinja hadi kwenye sehemu ya kuweka mizigo (Yard) na kuhakikisha kuwa kwa kushirikiana na wenzetu baada ya miezi mitatu hadi minne njia hii inaanza kufanya kazi" alisema Bwana Ruzigye

Mkuu wa Usafirishaji WFP Tanzania Ndugu Mahmudu Mabuyu amesema kuwa kufunguliwa kwa njia na Bandari ya Jinja kutasaidia kusafirisha kwa urahisi mizigo ya WFP pamoja wafanyabiashara wa Tanzania na Uganda .

# UJENZI WA MAHANDAKI RELI YA KISASA WAANZA RASMI MKOANI MOROGORO

Na Mwandishi wetu, TRC



Meneja Mradi Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Morogoro - Makutupora Mhandisi Faustine Kataraiya akitoa ufafanuzi kwa Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Atashasta Nditiye (wa tatu kulia) kuhusu hatua za uchorongaji Mahandaki yatakayopitisha reli ya kisasa eneo la Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Julai 2019.

Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye azindua rasmi uchorongaji Milima kwa ajili ya ujenzi wa mahandaki 'tunnels' yatakayopitisha reli ya Kisasa – SGR kipande cha Morogoro – Makutupora katika eneo la Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Julai 2019.

Jumla ya Mahandaki 4 yenye jumla ya urefu wa Kilometa 2.6 yanatarajiwa kujengwa katika Mradi wa SGR kipande cha Morogoro – Makutupora katika eneo la Kilosa ambapo handaki refu zaidi nchini linatarajiwa kujengwa likiwa na urefu wa Kilometa 1.031 sambamba na mahandaki mengine matatu ambayo yote kwa pamoja yataunganishwa na madaraja makubwa ili kuepusha athari za mafuriko ya mto mkondoa.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Mbunge wa Kilosa, Menejimenti na Wafanyakazi wa TRC na Yapi Merkezi, wanahabari pamoja na wananchi wa wilaya ya Kilosa katika Milima ya Kilosa mkoani Morogoro.

Waziri Nditiye ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo ameipongeza menejimenti na wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania kwa Usimamizi mzuri wa Miradi na kuwataka waendelee kuchapa kazi ili kuleta tija na matokeo mazuri katika utoaji huduma bora za usafiri wa reli.

Aidha Naibu Waziri amewashukuru wananchi wa mkoa wa Morogoro kwa ushirikiano wanaoutoa kwa wakandarasi na TRC, pia amewatoa hofu wananchi ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa kuwa endapo serikali itahitaji eneo kwa ajili ya ujenzi, mwenye eneo atalipwa fidia pamoja na stahiki nyingine anazostahili kulipwa.

"Napenda niwahakikishie watanzania, kwa Yule ambaye tutamfuata kwenye eneo lake tutamlipa fidia yake" Amesema Mhe. Atashasta

Reli na Matukio Gazeti
Toleo Namba 1, Ukurasa namba 6.







Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanznia Mhe, Dkt. John Pombe Magufuli akipata ufafanuzi kuhusu Maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa alipotembelea banda la TRC katika Maonesho ya 4 ya Viwanda na Biashara ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika - SADC katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa J.K Nyerere jijini Dar es Salaam Agosti 2019



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Shirika la Reli Tanzania - TRC Bi Jamila Mbarouk akifafanua jambo kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alipotembelea banda la TRC katika Maonesho ya 4 ya Viwanda na Biashara ya Jumuiya ya Nchi a Kusini mwa Afrika - SADC katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu J.K Nyerere jijini Dar es Salaam Agosti 2019.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (wa pili kulia) akipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa Mawasiliano na Ishara Bwana John Mandari kuhusu vifaa vya mawasiliano vilivyokuwa vikitumika katika shughuli za uendeshaji wa treni katika banda la TRC viwanja vya maonesho ya 43 ya kimataifa ya biashara - Sabasaba jijini Dar es Salaam Julai 2019.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe akishuka katika treni ya uhandisi ya Mkandarasi Yapi Merkezi baada ya kiufanya jaribio la kwanza la treni kupita juu ya reli eneo la Soga mkoani Pwani Julai 2019.



Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Atashasta Nditiye wa sita kulia akikata utepe kuashiria kuanza rasmi kazi ya uchorongaji mahandaki yakayopitisha reli ya kisasa - SGR eneo la Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Julai 2019.

# UBORESHWAJI WA RELI YA KATI KUWA CHACHU YA MAENDELEO TANZANIA

Na Mwandishi wetu, TRC



Maendeleo ya nchi yanakuja kama serikali imejiwekea mikakati mizuri na ambayo inalenga kujikwamua kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine kwa kutumia rasilimali zilizopo kuhakikisha taifa linapiga hatua na watu wake wanaondokana na hali duni ya maisha ambayo ndio chanzo cha umasikini miongoni mwa jamii ya watanzania, ungana na mwandishi wetu kukujuza zaidi juu ya swala hili la maendeleo ya kiuchumi pamoja na miundombinu.

Kwa bahati nzuri taifa hili limejaaliwa kuwa na kila aina ya rasilimali ikiwemo za madini, gesi, misitu, wanyama, na rasilimali nyingine, pia Serikali imekua ikijitahidi kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi pamoja na maendeleo ya miundombinu ambapo kwa sasa uchumi unakua kwa kasi.

Kipindi cha nyuma maendeleo ya miundombinu yalionesha kuleta kikwazo katika ukuaji wa uchumi wa nchi, ila kwa sasa serikali imekua ikitilia mkazo nyanja mbalimbali katika uboreshwaji wa miundombinu ikiwemo uboreshwaji wa reli ya kati kwa ajili ya kuimarisha huduma za usafiri wa mizigo na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania imekusudia kufanya ukarabati wa reli ya kati ili kurejesha ufanisi wake baada ya ufanisi wa reli hiyo kushuka kwa kiwango kikubwa katika utoaji wa huduma za ubebaji wa mizigo.

Kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia, mradi huo wa reli ya kati unaojulikana kwa jina la 'Tanzania Intermodal and Rail Development Project' (TIRP) ambao umekua na faida kubwa katika ukuzaji wa uchumi wa nchi, kwa kuleta fursa mbalimbali ikiwemo kuwepo kwa ajira na kujengewa ujuzi kwa wote watakaoshiriki shughuli a ujenzi na pia kukua kwa kipato cha wananchi kwenye maeneo ya mradi.

Pamoja na hayo kukamilika kwa mradi huo wa uboreshwaji wa reli ya kati, kutaboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji wa mizigo kwa miundombinu ya reli na madaraja, kuongezeka kwa mwendokasi wa treni kutoka kilometa 30 kwa saa hadi kufikia kilometa 70 kwa saa hivyo kupelekea kupunguza gharama za safari na usafirishaji, pia kupunguza muda wa kupakia na kupakua mizigo.

Vilevile mradi huu utaleta chachu katika kupunguza gharama za matengenezo ya barabara na serikali kuelekeza bajeti zaidi kwenda kwenye huduma nyingine za kijamii na kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa reli hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Hivi karibuni Serikali ilifanya ufunguzi wa reli ya Tanga hadi Moshi mkoani Kilimanjaro ulioambatana na uzinduzi wa treni za mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam na Tanga kuelekea Moshi mkoani Kilimanjaro chini ya Shirika la Reli Tanzania - TRC ambapo timu ya kutekeleza mradi huo ilijumuisha wafanyakazi wapatao 525 kutoka TRC, kati ya hao vibarua ni 466, wahandisi 12, na mafundi wa reli na nyanja nyingine 47.

Mkurugenzi mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa katika hafla hiyo amebainisha kuwa juhudi za Serikali na kujituma kwa wafanyakazi wa TRC kutafungua fursa mpya katika usafirishaji na uchukuzi katika ukanda huo wa Kilimanjaro ambapo historia inaonesha miaka 12 iliyopita Shirika lilikuwa na uwezo wa kusafirisha mazao mbalimbali tani elfu 70 kwa mwaka kutoka Tanga, tani laki moja za mbolea kwa mwaka na maharage mabehewa 144 kwa mwaka.

"Ningependa kuihakikishia Serikali kuwa Shirika la Reli Tanzania litaendelea kusimamia miradi yote ya kuboresha huduma za Shirika, utendaji na miundombinu kwa kasi na ubunifu " amezungumza Ndugu Kadogosa.

Hata hivyo Uboreshwaji wa Reli ya kati utatengeneza mpango endelevu wa miundombinu hasa ya reli kuwa na uhakika sio tu katika usafiri wa abiria bali na kufanya usafirishaji wa mabehewa ya mizigo kuwa ya ufanisi na haraka katika kukuza uchumi wa nchi.

>> Inaendelea Uk. 9

>> Inatoka Uk. 8

Vilevile uboreshwaji wa Reli hiyo utaleta faida kubwa kwa wafanyabiashara watakaotumia njia ya reli kwa kusafirisha mizigo kwa kupata gharama nafuu za usafirishaji wa mizigo na usafiri wa kuaminika, pia fursa za ajira zitaongezeka katika tofauti ndani ya shirika mara baada ya mradi kukamilika ili kuboresha huduma kwa wadau wa usafiri wa reli nchini.

Watanzania wanapaswa kuendelea kumuunga mkono Rais wa Jmhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe katika utekelezaji wa miradi mikubwa inayoendelea na kuilinda miradi aliyokamilika ili kuleta mapinduzi katika sekta ya reli, kuleta chachu katika uchumi nchini na kuiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

## UJENZI WA RELI YA KISASA SGR UTAKAVYO WAFAIDISHA WATANZANIA

Na Mwandishi wetu, TRC




Serikali ya awamu ya tano kupitia Shirika la Reli Tanzania – TRC wamekua kipaumbele katika kuhakikisha uboreshwaji wa njia za reli pamoja na ujenzi wa reli wa reli ya kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR) unakua kwa kiwango cha juu zaidi na kwa kasi ili nchi kufikia uchumi wa kati na kuboresha maisha ya watanzania. Reli ya kisasa – SGR ni reli ya kwanza Afrika Mashariki na kati itakayokuwa na uwezo wa kupitisha treni zitakazoendeshwa kwa nguvu ya umeme na yenye mwendo kasi usiopungua kilometa 160 kwa saa.

Ujenzi wa reli ya kisasa una mtandao usio pungua KM 2,561 ambao unajengwa kwa awamu tano ambazo ni Dar es Salaam – Morogoro km 300, Morogoro - Matukupola KM 422, Matukupola – Tabora KM 294, Tabora – Isaka KM 130, Isaka – Mwanza 249.

Mnamo tarehe 12 mwezi wa April, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli alizindua Ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro KM 300, ambao unaendelea na umefikia zaidi ya asilimia 60. Vilevile Tarehe 14, mwezi Machi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli alizindua Ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa kipande cha Morogoro - Matukupola KM 422, ambao umefikia zaidi ya asilimia 14.

Ujenzi wote wa awamu zote mbili upo chini ya kampuni ya ukandarasi YAPI MARKEZI kutoka nchini Uturuki.

Lengo kubwa la ujenzi wa reli ya kisasa ni kuongeza ufanisi katika uchukuzi na usafirishaji nchini hususani katika sekta ya reli.

Watanzania watafaidika na mradi huu wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi kukamilika, ambapo fursa nyingi zitapatikana kiuchumi ambazo ni kutoa njia ya haraka kwa ufanisi na uhakika, treni za kisasa zitaweza kupunguza mrundikano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam kwa kuhakikisha mizigo inayowasili bandarini na itasafirishwa bila kuchelewa.


>> Inaendelea Uk. 10

>> Inatoka Uk. 9

kukuza vipato vya wananchi ambao wanashiriki katika kutoa huduma mbalimbali katika mradi. Pia kuchangia katika pato la taifa na sera ya viwanda, mradi umeongeza mahitaji makubwa ya saruji na nondo pamoja na vifaa vingine vya ujenzi hivyo kuvifanya viwanda vya ndani kupata soko la bidhaa zake.

Hata ivyo Sekta ya usafirishaji pia imefaidika kwani kuna baadhi ya watanzania wamekodisha magari yao pamoja na kushiriki moja kwa moja katika usafirishaji wa vifaa na mitambo mbalimbali. Vilevile Sekta ya ujenzi, wakandarasi, wazawa wanashiriki moja kwa moja kutoa huduma za kandarasi za ujenzi. Faida za mradi huu kijamii ni ongezeko la ajira kwa wazawa kutoka sekta na fani mbalimbali. Pamoja uboreshwaji wa huduma za kijamii ikihusisha ujenzi wa shule, vituo vya afya, na ujenzi wa barabara katika maeneo yapitiwa na mradi.

Ujenzi wa reli ya kisasa utakapokamilika hasa wakati wa utendaji utakuwa na faida kiuchumi hasa ongezeko la usafirishaji wa mizigo ambapo reli itabeba mzigo hadi tani 10,000 kwa mkupuo sawa na Malori 500 ya mizigo. Uokoaji muda wa kusafiri kwa abiria na mizigo, kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Kuchochea maendeleo katika sekta ya kilimo, biashara, madini na viwanda hususani maeneo ambapo reli itapita pamoja na nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda, DRC na Kenya.



Daraja la Treni lenye urefu wa KM 2.6 linalojengwa kuanzia stesheni ya Dar es Salaam hadi Ilala jijini Dar es Salaam

Pia reli itasaidia kupunguza gharama za mara kwa mara za matengenezo ya barabara. Kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kupunguza muda wa safari mathalani Dar es salaam – Morogoro safari kuwa Saa 1 na Dakika 15, safari ya Dar es Salaam – Dodoma kutumia muda wa Saa 3. Kupunguza gharama za usafirishaji mizigo, inategemewa mara mradi utakapoanza gharama za usafirishaji wa mizigo itashuka kwa asilimia 40% na kuifanya bandari ya Dar es Salaam kuwa na ushindani.

Reli itasaidia kuchochea uanzishwaji wa viwanda katika maeneo mengine ya nchi, mradi utatoa uhakika wa usafirishaji wa malighafi na bidhaa na kuipatia fursa nchi kwenye uwekezaji wa miradi kwa kuweesha mazingira ya uwekeaji ikiwa ni pamoja na miundombinu imara.

Kuwa sehemu ya uanzishwaji wa miji midogo, sehemu zinazojengwa stesheni huwa zinaongeza chachu ya uanzishwaji wa makazi ya watu kutokana kuwa na uhakika wa usafiri. Maeneo ya Soga, Ruvu na Kwala kwa Mkoa wa Pwani yatumike kupanga makazi ya watu na itaiongezea reli faida ya abiria na mizigo.

Pia itaongeza soko la ndani na kuimarisha Shilingi ya Tanzania (economy localization) hii ni kutokana na treni kutumia umeme utakaozalishwa nchini, kama tungetumia mafuta ambayo ni lazima kuagiza ingeongeza gharama kubwa kwa uendeshaji na pia matumizi ya akiba ya fedha za nje na kutoa ajira.

Hivyo hivyo Kijamii reli ikikamilika itapunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya magari makubwa kwenye barabara na kupelekea kupunguza ajali na kufanya barabara kuwa njia salama zaidi ya usafiri. Pia Serikali itaweza kuboresha huduma za kijamii kwa kutumia pesa ambazo zingetakiwa kufanya matengenezo ya barabara ambazo zingeharibika kutokana na mzigo mkubwa.

Hivyo basi watanzania kwa ujumla wanao wajibu wa kuilinda na kuitunza miundombinu ya reli kwa manufaa ya maendeleo ya nchi na ukuzaji wa uchumi, hili litahamasisha na kuchochea ukuaji wa kibiashara na viwanda pamoja na kuongeza mapato ya kodi nchini.

## Usalama Kwanza

# Uonapo Alama hii

# Simama

## Angalia kushoto na kulia kabla ya kukatiza/kuvuka reli.




Shirika la Reli Tanzania - TRC linawatangazia wananchi wote wanaoishi kandokando ya reli ya Tanga - Moshi mkoani Kilimanjaro kuwa kuanzia Julai 20, 2019 Shirika litaanza huduma ya usafirishaji wa Mizigo ikifuatiwa na huduma ya treni za abiria ifikapo mwezi
Septemba, hivyo wananchi wa Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro wanaoishi maeneo yanayopitia reli wanaombwa kuwa waangalifu pindi wanapokatiza reli na wanapaswa kuchukua tahadhari ikiwemo kufuata sheria na taratibu za usalama wa reli pindi wanapokatiza reli.

TRC Zijue Alama za Reli

### Hakikisha Unazingatia Tahadhari


za kiusalama kabla ya kuvuka/Kukatiza reli, ni Muhimu.



TRC Zijue Alama za Reli

### Dereva Hakikisha

Chombo chako (Gari/Pikipiki) kinakuwa umbali wa Mita 3.5 kutoka relini endapo utasikia honi ya treni.




TRC Zijue Alama za Reli

### Usikiapo Honi ya Treni Simama

Usivuke/Kukatiza reli mpaka treni itakapopita



Si Salama kutembea ama kuendesha chombo cha moto kwenye njia ya reli.



# Reli na Matukio Gazeti

## NENO LA SHUKRANI KWA WANANCHI WA TANGA, MOSHI NA ARUSHA

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania – TRC ndugu Masanja Kungu Kadogosa atoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Tanga, Moshi na Arusha kwa kujitokeza kwa wingi katika hafla ya ufunguzi wa reli ya Tanga mpaka Moshi/ Kilimanjaro iliyofanyika mjini Moshi Kilimanjaro Julai 20, 2019.

Ndugu Kadogosa amesema kuwa kujitokeza huko ni ishara tosha inayoonyesha kupenda na kukubali maendeleo ya nchi ya Tanzania yanayoendelea kufanyika na hasa katika uboreshaji wa miundombinu ikiwemo reli.

Pia Ndugu Kadogosa amewapongeza wafanyakazi wa Shirika la Reli – TRC kwa uzalendo na juhudi kubwa walizozifanya katika mradi wa ufufuaji wa njia ya reli kutoka Tanga hadi Moshi pamoja na kuihakikishia serikali kuwa TRC litaendelea kusimamia miradi yote ya kuboresha huduma za Shirika, utendaji na miundombinu kwa kasi na ubunifu kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.




**NDUGU MASANJA KUNGU KADOGOSA**
**MKURUGENZI MKUU SHIRIKA LA RELI TANZANIA - TRC**

Mkurugenzi Mkuu ndugu Kadogosa amewaasa wananchi wa Tanga, Moshi na Arusha kuchukua tahadhari wanapovuka kwenye makutano ya reli na njia nyingine na pia kushirikiana kwa pamoja katika kuilinda miundombinu ya reli ili Shirika liendelee kutoa huduma bora.

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| MHARIRI MKUU | MHARIRI MSAIDIZI | MTAYARISHAJI | MAKALA | HABARI | PICHA |
|---|---|---|---|---|---|
| Jamila Mbarouk | Mohammed Mapondela | Sami Omary | Aziza Charles | Tracy Robert | Musa Kadiko |

Kwa Maelezo zaidi piga Simu ya Bure 0800 11 00 42 au tembelea www.trc.co.tz

tzrailways TRC Reli TV Reli Yetu, Maendeleo Yetu, Taifa Letu #TRCMpya